# OFISI YA WAZIRI MKUU
# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI | www.pmo.go.tz | DODOMA | TOLEO LA NOVEMBA 2022




**Katibu Mkuu**
**Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu**
**2 Barabara ya Posta 40412 Dodoma Tanzania**




# Serikali yalenga kuimarisha usawa mapambano virusi vya UKIMWI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amepongeza Tume ya kudhibiti UKIMWI, Wizara ya Afya na Wizara ya TAMISEMI katika Mkakati wa kupambana na Ukimwi kama janga la kitaifa.

Hayo yamesemwa Waziri na Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene Jijini Dar es saalam, wakati wa uzinduzi wa taarifa ya hali ya UKIMWI duniani yenye Kauli Mbiu inayosema Dangerous Inequalities iliyotolewa Mkurugenzi Mtendaji anayeshughulikia Ukimwi Duniani UNAIDS Bi, Winnie Byanyima.

“Serikali imedhamiria kuweka usawa wa kijografia usawa kimazingira usawa kati ya watoto na wakubwa na usawa wa kiuchumi ili kuhakikisha watu wote wanapata huduma sawa ili wasiathirike na wale walio athirika wapate huduma za matibabu lakini pia huduma sawasawa kuhakikisha wanaendesha maisha yao.”

Akitoa taarifa hiyo Mkurugenzi Mtendaji anayeshughulikia Ukimwi Duniani UNAIDS Bi, Winnie Byanyima amesema Tanzania imejitahidi kupunguza Ongezeko la Maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kila Mwaka kwa miaka kumi mfululizo.

“Tanzania Imejitahidi kupunguza vifo vinavyosababishwa na UKIMWI na imekuwa ikifanya vizuri katika mapambano dhidi ya virusi vya UKIMWI.”

# MATUKIO KATIKA PICHA BUNGENI DODOMA



**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. George Simbachawene (kushoto) pamoja na Naibu Waziri TAMISEMI Mhe. David Silinde (kulia) wakitoka nje ya Ukumbi wa bunge.**



**Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga akiwa katika picha ya pamoja na Mbunge wa Jimbo la Mchinga Mhe. Salma Kikwete mara baada ya kushiriki katika vikao vya bunge vinavyoendelea Jijini Dodoma.**



**Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga akisalimiana na Mbunge viti maalum Mhe. Shally Raymond katika viwanja vya Bunge Dodoma.**



**Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Ummy Nderiananga akiwa pamoja na mwanafunzi wa Chuo kishirikishi cha elimu Dar es Salaam (DUCE) Bi. Chrisanta Gervas nje ya ukumbi wa Bunge.**




# Waziri Simbachawene, ahimiza mafunzo ya itifaki kuwa endelevu

Waziri wa Nchi wa Ofisi ya Waziri Mkuu sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene amesema ipo haja, mafunzo ya itifaki na uratibu wa maadhimisho kufanyika kila mwaka.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Mhe. George Simbachawene wakati akifunga mafunzo kwa watendaji wa serikali yaliyohusu itifaki ya viongozi wa kitaifa iliyowakutanisha Wakurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu na Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa yaliyofanyika Mkoani Singida

"Mafunzo haya yanapaswa kuongezwa mada na kuongeza namba ya washiriki ili kujenga uelewa wa pamoja"

Ambao utasaidia kupata ufahamu na ujuzi muhimu wa namna ya uandaaji wa Maadhimisho yanayohusu Idara na Taasisi za Serikali kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kuzijua kanuni za kiitifaki ambazo mtazitumia katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali kwenye taasisi zenu.

Awali Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya waziri Mkuu Sera Bunge na Uratibu Bwn. Kaspar Mmuya amesema mafunzo yamelenga kuwa na utaratibu ambao umekubaliwa, ambao unaleta matokeo chanya na watu wote kuheshimu.

"Watendaji waliopokea mafunzo sasa watasaidia katika maeneo yao; kitengo cha maadhimisho Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu ndio Ofisi inayosimamia itifaki za viongozi".

Naye Mtendaji Mkuu wa Mahakama Tanzania Profesa Elisante Ole Gabriel aliyekuwa mtoa maada wa huduma bora kwa mteja; ameshukuru serikali kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yamesaidia kuwajenga watendaji kwenda kwa muelekeo unaolengwa na nchi.

"Huu ni uwekezaji wa kifikira unaofaa, watendaji wakitoa huduma bora kwa wananchi na kwa viongozi, mashauri yatapungua kwa sababu ya huduma kuwa nzuri."



# Mhe. Katambi: Endeleeni kuchangia mfuko wa udhamini wa kudhibiti UKIMWIMhe. Katambi: Endeleeni kuchangia mfuko wa udhamini wa kudhibiti UKIMWI

Naibu Waziri Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Patrobas Katambi ameiasa jamii na wadau kuendelea kuchangia fedha katika mfuko wa udhamini wa kudhibiti UKIMWI (ATF) ili kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za afua za UKIMWI nchini.

Ameyasema hayo tarehe 27 novemba, 2022 wakati akihutubia kwa niaba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa kwenye Shughuli za mbio za nyika (Marathon) za kuchangia mfuko huo kwa kuanzia Uwanja wa Ilulu na kumalizikia katika uwaja huo kwa kukimbia kilomita 21,10 na 5 zilizowakilisha taswira ya utayari wa kila mmoja wetu kuchangia mfuko huu kwa hali na mali.

Alisema kustawi kwa mfuko huu kutasaidia kupunguza utegemezi wa rasilimali fedha kutoka kwa wahisani wa nchi za kigeni na kueleza kuwa uwepo wa mfuko imara unatupa uhakika wa uendelevu wa afua za UKIMWI nchini.

Mhe. Katambi aliwapongeza washiriki wote wa mbio hizo huku akotoa rai kwa jamii kuendelea kujitokeza kuchangia mfuko huo kuwa na uhakika wa fedha katika utekelezaji wa afua za masuala ya UKIMWI.

"Kipekee, niwashukuru Wadhamini na Washiriki wote wa Mbio hizi za ATF Marathon 2022 Lindi. Asanteni sana kwa kuchangia Mfuko huu na kushiriki mbio hizi za Marathon, natoa wito kwa Makampuni, Asasi mbalimbali na wananchi wote kuendelea kuhamasika kuchangia mfuko wetu kupitia akaunti ya Benki namba 20110033895 iliyopo Benki ya NMB na namba za simu ya mkononi 0684 90 90 90 kwa ajili ya kuboresha na uendelevu wa huduma za kudhibiti VVU na UKIMWI na hivyo, kuimarisha afya na kuokoa maisha ya Watanzania," Alisisitiza Mhe. Katambi

Alifafanua kuwa, Serikali inauchukulia kwa uzito mkubwa Mfuko huu na kuahidi kuendelea kushirikiana na Wadau wote ili kuona namna bora, endelevu na ya uhakika ya kutunisha mfuko huu.

Aidha, Mfuko huo ulianzishwa takribani miaka Saba iliyopita na yamepatikana mafanikio makubwa sana kwani umeweze kukusanya jumla ya Sh. 4,993,373,407.24.

"Fedha hizi zimesaidia sana kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI ikiwemo ununuzi wa dawa za magonjwa nyemelezi kwa WAVIU ambapo kiasi cha Shs Billioni 1.56 zilitolewa kwa Wizara ya Afya kusaidia upatikanaji wa Dawa hizo," alisema

Sambamba na hilo, Mfuko umesaidia ujenzi wa upanuzi wa Kituo cha Afya Mererani (Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro) ambacho licha ya kutoa huduma nyingine za afya, kituo hiki kinatumika kutoa huduma za dawa za kufubaza VVU yaani ARV kwa WAVIU na kuwa kitovu cha uelimishaji wa wananchi kujiepusha na maambukizo mapya ya VVU, ambapo kiasi cha Shilingi milioni 245 zilitumika.




# Serikali yajidhatiti kutokomeza maambukizo mapya ya VVU

Serikali imedhamiria kutokomeza maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI nchini kwa kuweka mikakati madhubuti ili kufikia malengo hayo ifikapo 2030.

Hayo yamesemwa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera Bunge na Uratibu Bw. Kaspar Mmuya wakati akifungua Mkutano wa mwaka wa vijana, viongozi wa dini na wadau wanaotekeleza miradi ya vijana balehe na wanawake vijana katika ukumbi wa Sea View Beach Resort mkoani Lindi tarehe 25 Novemba, 2022 katika kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani.

Kongamano hilo la siku mbili limebebwa na kaulimbiu inayosema; "Imarisha Usawa, Kujilinda ni ibada"

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema kuwa, katika kuyafikia malengo ni lazima kuwe na mikakati madhubutu inayotekelezeka ili kuhakikisha changamoto ya maambukizi mapya inakwisha nchini ifikapo 2030.

"Ifikapo mwaka 2030 tunapaswa kutokuwa na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI na kuhakikisha hakuna atakayepoteza uhai kwa ugonjwa huo pamoja na kutokomeza unyanyapaa pamoja na jitihada zingine tunaendelea kuwa na mikakakati mbalimbali ya kuweza kutambua afya za watu kwani ni zaidi ya watu milioni moja na laki saba wanaoishi na maambukizi ya UKIMWI,"alisisitiza Mmuya.

Aidha alisema kuwa serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU zinaendelea kupatikana kwa wingi na kwa wakati ili kila mmoja aendelee kuwa na afya njema na kulitumikia taifa letu. Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini Dkt. Leonard Maboko akieleza mikakati ya Tume hiyo katika kupambana na maambukizi mapya alisema, kundi kubwa linaloongoza katika maambukizi mapya ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 nchini . katika maambukizi mapya ni pamoja na; vijana kuendeleza mapenzi katika umri mdogo, kukosa malezi mazuri, kuendekeza mihemko na kuwa na mahusiano na watu wenye umri mkubwa pamoja na hali duni ya uchumi.

"Tabia ya kuendekeza ngono maarufu kama kupiga shoo na kupenda masponsor, hii inakwamisha jitihada za Serikali katika mapambano haya kwani vijana wameendelea kuishi na kufuata tabia hizo na kusahau tabia njema ya kumcha Mungu inazowasaidia wengi katika kushinda tamaa za ujana,"alisema Dkt. Maboko

Aliongeza kuwa, pamoja na takwimu hizo bado Serikali haijaacha kuwa na mikakati mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa kutoa fursa kwa vijana kuondokana na changamoto zao ikiwemo za kiuchumi.

“Kongamano hili limehusisha vijana na viongozi wa dini kwa kuzingatia mchango wao katika kuendelea kusaidia mapambano haya ikiwa ni pamoja na kukemea matukio ya unyanyapaa na kuhimiza matumizi ya ARV kwa wanaogundulika kuwa na maambukizi huku wakihimiza vijana kuendelea kumcha Mungu na kujitenga na uovu “alisisitiza Dkt Maboko.

Jarida hili la Mtandao limeandaliwa
na kutolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Bunge na
Uratibu

KATIBU MKUU
Ofisi ya Waziri Mkuu
2 Mtaa wa Relini, S. L.P 980
40480 Dodoma,
Barua pepe;ps@pmo.go.tz, Simu;+255262322480
Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz